Barua hii imekusudiwa kwa familia ambazo:

- Watoto waliopokea udhamini wa chakula wa SNAP Machi 2020.
- Watoto ambao wameidhinishwa kupokea chakula shuleni bila malipo au kwa bei iliyopunguzwa kipindi cha 2019-20 mwaka wa shule Texas.
- Watoto ambao huhudhuria shule ambazo zinawapa wanafunzi wote chakula bila malipo (Bidhaa kwa Jamii zinazostahili au Bidhaa 2).

Ikiwa hutimizi angalau kigezo kimoja kati ya hizi, hustahili udhamini uliolezewa hapa chini.

Mpendwa Mzazi au Mlezi,

Tunaelewa unapitia hali ngumu na tungependa ujue kwamba huenda familia yako inastahili kupokea Udhamini wa Janga wa Kielektroniki (P-EBT) ili kununua chakula kutoka kwa muuzaji anayekubali Kadi ya Texas Lone star.

P-EBT ni udhamini wa mara moja wa hadi $285 na utapeanwa kupitia kadi ya EBT ili kusadia familia katika kipindi hiki ambacho shule zimefungwa bila kutarajiwa.

Watoto wa hadi umri wa miaka 21 ambao wameidhinishwa kupokea chakula bila malipo au kwa bei iliyopunguzwa shuleni Texas katika kipindi cha mwaka wa shule 2019-20 na watoto wote ambao huhudhuria shule ambayo huwapa wanafunzi wote chakula bila malipo (Bidhaa kwa Jamii zinazostahili au Bidhaa 2) wanastahili kupokea udhamini wa P-EBT.

Familia ambazo zilipokea udhamini wa SNAP mwezi wa Machi 2020 na wana watoto wa umri wa miaka 5-18 kuanzia Mei 17, 2020, hawahitaji kutuma maombi kwa ajili ya watoto hao. Familia hizi zitapokea udhamini P-EBT kwenye Kadi yao ya Lone Star ya sasa kufikia Mei 22. Huhitaji kufanya jambo lingine lolote.

Familia zilizo na watoto walio na hadi umri wa miaka 21 ambao wameidhinishwa kupokea chakula bila malipo au kwa bei iliyopunguzwa kipindi cha mwaka wa shule 2019-20 wanahitaji kutuma maombi ya P-EBT. (Hii inajumuisha familia ambazo zilipokea udhamini wa SNAP mwezi wa Machi 2002 na wana watoto wenye umri wa chini ya miaka 5 na kati ya 19 na 21.) Familia hizi zitahitaji kutuma maombi ya P-EBT kwenye mtandao. Familia zinazostahili zitapokea barua pepe iliyo na linki ya ombi la P-EBT wiki ya kwanza ya Juni. Utakuwa na hadi Juni 30, 2020 kujaza ombi. Mara tu itakapoidhinishwa, familia yako itatumiwa kadi ya P-EBT kupitia barua.

Tafadhali rejelea kitini cha "Jinsi ya kutuma maombi ya P-EBT" kwa habari zaidi kuhusu utaratibu wa kutuma maombi na habari utakayohitajika kutoa.

Utakuwa na mwaka mmoja, kutoka tarehe ya uliyopewa udhamini, kutumia udhamini wako wa chakula wa P-EBT. Udhamini wa P-EBT hauwezi kupeanwa kwa mtu mwingine.
Tunaamini kwamba udhamini huu utakuwa wenye msaada. Kwa habari zaidi, tafadhali tembelea hhs.texas.gov/PEBT. Kituo cha Kupiga simu cha P-EBT kinapatikana Juni wakati maombi yanapatikana. Nambari ya simu itajumuishwa kwenye habari tunayokutumia pamoja na linki ya maombi.

Mwaminifu,